**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNSI STADI**
**CHUO CHA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA TANGA**

Ili kufanikisha mafunzo ya ufundi kila mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria zifuatazo:-

**1. MAHUDHURIO:**

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni saa 1:30 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1:30 wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni. **Adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji**

(b) Mwanafunzi hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na mwalimu (mkuu wa sehemu)

(c) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike kwa mwalimu (mkuu wa sehemu) bila ya kufanya hivyo ni kosa.

(d) Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi hataruhusiwa kufanya mitihani yake ya kuhitimu.

**2. MAVAZI**

(a) Sare ya chuo ni suruali ya Bluu na shati jeupe la mikono mifupi. Sare hiyo ivaliwe siku za Jumatatu, Jumanne na Alhamisi, siku za Jumatano na Ijumaa Tshirt na suruali ya Blue zitavaliwa. Wakati wote shati liwe limechomekewa vizuri kwa mkanda.

(b) Ovaroll livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(c) Viatu vyenye visingino virefu na kandambili au viatu vya wazi (Sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni. Viatu vinavyokubalika ni vyeusi vyenye visigino vifupi na gidamu (kamba) na vivaliwe na soksi.

**3. USAFI WA MWILI**

(a) Hairuhusiwi kuvaa hereni, pete, bangili, mkufu na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.

(b) Nywele kwa wavulana

(i) Zikatwe ziwe fupi sana, **KIPARA** hakiruhusiwi kabisa.

(ii) Ndevu haziruhusiwi (Sharubu, sharafa na ndevu za kidevuni/kionja mchuzi)

(c) Nywele kwa wasichana

(i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma isiyopungua sita na kuzidi saba.

(d) Kucha zisifugwe kabisa wala kupaka rangi.

4. Wizi wa mali za chuo au mali ya mtu yeyote yule:-

(a) Vitendo vyovyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzake, hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

(b) Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakununue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.

(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyo ndani ya chuo. Kama itahitajika kwa mwanafunzi kuwa na kifaa cha aina tajwa, atatoa taarifa kwa mkuu wa sehemu kwa ajili ya utambuzi na kibali.

5. **Ugomvi:** Ugomvi, kupigana na kushambuliana ni kosa la jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

6. **Ulevi:** Iwapo itabainika mwanafunzi analewa, au kuonekana katika sehemu za kileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

7. **Mapenzi:** (a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.

(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike hairuhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.

8. **Migomo**: Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Atakayeshawishi au kusababisha migomo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

9. **Lugha:** Lugha inayotumika kuendesha masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingereza.

10. Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalumu kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja

11. Ni marufuku kuwasha simu za mkononi wakati wote wa vipindi

12. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya chuo siku zifuatazo:-

(i) Jumapili tangu saa 12:00 asubuhi hadi 12:00 jioni

(ii) Jumamosi tangu saa 7:00 mchana hadi saa 12:00 jioni
Hairuhusiwi kutoka nje ya chuo wakati wowote bila kibali maalumu.

13. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la chuo anapaswa kuwa na sare na kitambulisho cha chuo, atajiandikisha lango kuu la chuo. Mwanafunzi

atakayeonekena nje ya maeneo ya chuo bila kuwa na sare na kitambulisho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anwa nafasi ya kulala bweni au kufukuzwa chuoni.

14. Mwanafunzi atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya chuo bila kibali atasimamishwa masomo.

15. Haitaruhusiwa kupika chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.

16. (a) Ni marufuku wanachuo wa kiume na wa kike kutembeleana mabwenini.

    (b) Hairuhusiwi **KABISA** kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa chuo bila ruhusa au kibali.

17. Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu/mlezi itatolewa.

18. Taa za madarasani na mabwenini zizimwe saa 4:00 za usiku.

19. Hakuna ruhusa kumkaribisha au kumlaza mgeni, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.

    - Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 12:00 jioni

    - Kila Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni

20. Vyumba/madarasa na vifaa vitumike kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.

21. Hairuhusiwi kulala nje ya chuo. Iwapo ikitokea ruhusa itatolewa na ofisi ya Mkuu wa chuo.

22. Ruhusa ya kutoka chuoni; Jumamosi saa 7:30 mchana hadi saa 12:00 jioni. Jumapili na siku za sikukuu saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni; majina yaandikwe kwenye kitabu cha kutoka na kuingia. Mhusika aweke muda wa kutoka na kusaini arudipo.

23. Hairuhusiwi kabisa kwa mwanafunzi wa kutwa kwenda bwenini bila kibali maalumu.

24. Ni jukumu la kila mwanafunzi kufuata kwa makini ratiba ya chuo awe sehemu husika muda husika.

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNSI STADI
CHUO CHA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA TANGA

MALIPO YA ADA NA MICHANGO MBALIMBALI
YA CHUO

| **MWAKA WA KWANZA 2025** | | | |
|---|---|---|---|
| **A. ADA** | **KUTWA** | **BWENI** | **MAELEKEZO** |
| ADA YA MAFUNZO | **60,000.00** | **120,000.00** | **PATA CONTROL NUMBER** |
| **B. MICHANGO MINGINE** | | | |
| NEMBO YA VETA 2PC | 5,000.00 | 5,000.00 | **LIPA KWENYE CONTROL NUMBER UTAKAYOPEWA CHUONI** |
| TAHADHARI | 20,000.00 | 20,000.00 | |
| KITAMBULISHO | 5,000.00 | 5,000.00 | |
| MAHAFALI | 10,000.00 | 10,000.00 | |
| MICHEZO | 10,000.00 | 10,000.00 | |
| PICHA YA KITAMBULISHO | 1,000.00 | 1,000.00 | |
| FULANA YA CHUO | 15,000.00 | 15,000.00 | |
| **JUMLA MICHANGO MINGINE** | **66,000.00** | **66,000.00** | |
| **C. BIMA YA AFYA YA NHIF** | | | |
| **BIMA YA AFYA** (UNATAKIWA UJE NA KITAMBULISHO AU NAMBA YA NIDA KWA AJILI YA KUFANIKISHA MALIPO YA BIMA YA AFYA. MWANAFUNZI AMBAYE HATAKUWA NA KITAMBULISHO CHA NIDA AU NAMBA HATAPOKELEWA CHUONI). | 50,400.00 | **50,400.00** | **LIPA KWENYE CONTROL NUMBER UTAKAYOPEWA YA NHIF UFIKAPO CHUONI** |
| **JUMLA KUU** | | | |
| ***FANI*** | **KUTWA** | **BWENI** | **MAELEZO** |
| *FANI ZOTE ZA UHANDISI* | **146,400.00** | **176,400.00** | **NUSU MUHULA** |

| **D. SARE ZA CHUO (KILA MWANACHUO ATASHONA SARE KAMA ILIVYOAINISHWA HAPO CHINI)** | |
|---|---|
| *SURUALI 2PCS ZA DARK BLUE KWA KWA FANI ZOTE* | **RANGI YA KITAMBAA CHA KUSHONA SARE ZA CHUO YAANI SURUARI, KOTI NA OVERCOAT NO DARK BLUE.<br>VIPIMO VYA SURUALI KWA CHINI NI NCHI 14 NA KUENDELEA, SURUALI IWE NA MARINDA MAWILI KUSHOTO NA KULIA SIO MODO.<br>HAKIKISHA UNASHONA KWA VIPIMO NA RANGI HALISI YA KITAMBAA. VINGINEVYO HUTAPOKELEWA LAKINI PIA BAADA YA KUPOKELEWA KAMA UTAFANYA MAREKEBISHO YOYOTE KWENYE SARE ZAKO NA IKABAINIKA SARE HIYO ITACHANWA NA UTASIMAMISHWA MASOMO HADI UTAKAPOSHONA NYINGINE YENYE RANGI NA VIPIMO VILIVYOAINISHWA NA HATUA ZAIDI ZA KINIDHAMU ZITACHUKULIWA DHIDI YAKO.** |
| *COAT LA DARK BLUE KWA FANI YA UHAZILI NA KOMPYUTA* | |
| *MASHATI MAWILI (02) MEUPE MIKONO MIREFU KWA FANI ZOTE ZA UKARIMU.* | |
| *OVERALL NA VIATU VIGUMU VYA USALAMA KAZINI (SAFETY BOOT) KWA FANI ZA UHANDISI* | |
| *CHEF COAT/WAIST COAT, APRON, NECK TIE, KOFIA, KIZIBAO NA TORTION KWA FANI ZA UKARIMU* | |
| *SWETA LA DARK BLUE KWA MWENYE CHANGAMOTO YA AFYA. HAIRUHUSIWI KUVAA SWETA AU KOTI LA RANGI YOYOTE NJE YA DARK BLUE.* | |

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNSI STADI**
**CHUO CHA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA TANGA**

| | |
|---|---|
| | **ZINGATIA:-**<br>**HAKUNA MWANACHUO ATAKAYE POKELEWA BILA KUWA NA SARE ZA CHUO ZENYE RANGI NA VIPIMO HALISI PIA LAZIMA AWE NA KITAMBULISHO CHA NIDA AU NAMBA YA NIDA KWA AJILI YA BIMA YA AFYA.** |

**<u>ZINGATIA</u>**

- Kwa Mwanafunzi wa Bweni aje na godoro lake lenye size **2.5’** × **6’** × **3**” ambalo litakuwa mali yake mwenyewe pamoja na chandarua
- Kwa wanafunzi wa bweni waje na vyombo vya kulia chakula na ndoo mbili za maji ya matumizi.
- Kila Mwanafunzi aje na mashati mawili meupe ya mikono mifupi kwa fani za uhandisi, mashati mikono mirefu kwa fani za ukarimu, pia wanafunzi wa fani ya Uhazili na Kompyuta waje na koti la rangi ya blue.
- Kila mwanafunzi aje Soksi nyeupe jozi mbili
- Kila mwanafunzi aje na Madaftali makubwa (quire 2 au 3) 10
- Kila mwanafunzi aje na kalamu za wino pamoja na vifaa vya kucholea kwa fani za uhandisi na uhazili.
- Kila mwanafunzi aje na “REAM MOJA YA KARATASI” aina ya TOP KOPIE yenye kava la blue au No.1 yenye rangi ya njano.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNSI STADI**
**CHUO CHA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA TANGA**

The Medical Officer Date:
……………………
…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………….

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine the above candidate his/her fitness to undergo Training subsequently work as/an

……………………………………………………………………………………………………
……………………………………

i) Hearing
………………………………………………………………………………………………
………………………………

ii) Asthma
………………………………………………………………………………………………
……………………………...

iii) Other serious disease(s)
………………………………………………………………………………………

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit /unfit for training above.
**Date** …………………………………. **Designation** ……………………………. **Signature & Official Stamp.**
……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………

**KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**A. MWANACHUO**

Mimi ………………………………………………………………….……… ninakubali nafasi ya mafunzo kwa Fani niliyochagua na nitafuata Sheria za Chuo.
**Sahihi**: ………………………………………………………… **Tarehe** …………………………………………………..

**B. MDHAMINI**

Mimi ……………………………………………………………………. S. L. P …………….……………………
Ninathibitisha kuwa namdhamini aliyetajwa hapo juu nitamlipia gharama zote za Mafunzo (Ada) n.k. pamoja na nauli wakati wowote wa kwenda Chuoni na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo.
**Sahihi**: ……………………………………………………..…… **Tarehe** ………………………..…………………